## MWANDISHI



Kitabu hiki kimeandikwa na Moses Chai Mrima kama mwongozo wa ibada kwa wakristo wote. Mwandishi ni mzaliwa wa Chumani/ Ngerenyi, Kilifi North Sub County, Kilifi County. Wazazi wake ni Bw.Albert Jambo Charo na Florrence Mbuche Charo. Yuko na ndugu kadhaa. Alizaliwa mnamo mwaka wa 1975, January. Alioa kwenye ndoa katika kanisa la KAG, Kilifi, mwaka wa 2007, mkewe akiwa ni Triza Elavuna Chai, kutoka Kitale, ambaye pia ni Mwalimu wa Sekondari, Lamu County na Mhubiri wa Injili ya Yesu Kristo. Wamebarikiwa na watoto wawili kufikia sasa wakiwa ni Faith Mbuche Chai na Gift Elavuna Chai. Mwandishi alisomea shule ya msingi ya Chumani kutoka 1981 hadi 1988, ndipo akajiunga na shule ya upili ya Chumani mwaka wa 1989 hadi 1992. Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret , kwenye chuo chake shikilizi cha Maseno kuanzia 1994 hadi 1999, alipofuzu na Shahada ya Elimu, yaani B.Ed. Degree in Education. Mnamo mwaka wa 2015 alifuzu tena na shahada ya pili, ya uzamili kwenye Chuo Kikuu cha Kenyatta, yaani Masters' Degree in Education Planning. Saa hii anaendelea na kazi yake ya walimu akiwa Naibu wa Mwalimu Mkuu kwenye Shule ya Upili ya Mapunga, Tana Delta Sub- County, Tana River County, huku akiwa Mchungaji wa Kanisa.

Mwandishi alipakwa mafuta na Mchungaji Sara Kondo mwaka wa 2000, ili kuwa Mchungaji Msaidizi kwenye kanisa la Ahadi Worship Centre, Mkunguni/Chumani, Kilifi County. Baada ya huduma ya Ahadi Gospel Ministry kusajiliwa na serikali mwaka wa 2013, aliwekwa wakfu(ordained) kuwa Askofu mwaka wa 2016, akiwa chini ya Askofu Mkuu Sara Kondo.

Akiwa askofu, ni Mchungaji wa Makanisa ya Ahadi Gospel Ministry yanayopatikana sehemu za Chumani,Ngerenyi, Roka, Kilifi Town, Matanomanne/ Vitengeni katika Kilifi County, na Chakamba, Tana Delta Sub County, Tana River County.

Maono ya huduma ni kuendelea kumhubiri Yesu Kristo hadi atakaporudi kwa mara ya pili na kupanua mipaka ya kazi hali tukimngojea kurudi.

# AHADI GOSPEL MINISTRY
# KILIFI/ KENYA

# Mwongozo wa Ibada za Kikristo

### Kimetayarishwa na

### Bishop Moses Chai Mrima

© 2016





## YALIYOMO


YALIYOMO ........ i

UTANGULIZI ........ ii

MAWAIDHA KUMI-wachungaji wana shughuli nyingi lakini zingatia: ........ iii

1.0. IBADA YA UBATIZO WA MAJI MENGI ........ 1

1.1 Hatua za Kufuata ........ 1

2.0. IBADA YA MEZA YA BWANA ........ 1

2.1. Hatua za Kufuata ........ 1

3.0. IBADA YA NDOA ........ 2

3.1. Hatua za Kufuata ........ 2

4.0. IBADA YA MAZISHI ........ 5

4.1. Hatua za Kufuata ........ 5

5.0. IBADA YA KUOMBEA WATOTO ........ 6

5.1. Hatua za Kufuata ........ 6

6.0. IBADA YA KUONDOA NADHIRI ........ 6

6.1. Hatua za kufuata ........ 6

7.0. IBADA YA KUWEKA WAKFU/ KUSIMIKA WAHUDUMU (ORDINATION) ........ 7

7.1. Hatua za Kufuata ........ 7

8.0.IBADA YA KUWEKA WAKFU KANISA ........ 7

8.1.Hatau za Kufuata ........ 7

9.0.IBADA YA USHIRIKA WA JUMAPILI KANISANI ........ 8

9.1.Hatua za Kufuata ........ 8

10.0.IBADA YA USHIRIKA WA KATIKATI YA WIKI ........ 8

10.1.Hatua za Kufuata ........ 8

USHAURI WA MWISHO ........ 8

# UTANGULIZI

Ibada ni sehemu muhimu sana katika huduma ya Mchungaji na mara nyingi sana watu huamini kwamba mtumishi akiwepo basi kila kitu kiko salama. Hata hivyo, imekuwa changamoto kubwa sana kwa wachungaji wengi maana uzoefu wa kuendesha ibada hizo ni haba ama duni. Hii imesababisha wachungaji kukosa ujasiri wanapotekeleza majukumu yao. Kitabu hiki kimetayarishwa ili kusaidia mahali fulani katika kujenga ujasiri wa wachungaji kwa kutoa mwelekeo kwa ibada tofauti tofauti. Mchungaji anaweza kufanya marekebisho mahali ambapo anaona umuhimu wa kufanya hivyo. Ujumbe huu umelenga wachungaji wote wa kanisa la Yesu Kristo na wala sio dini au huduma fulani.



- Kutoa Shukrani
- Sadaka
- Kufunga kwa Maombi

**9.0.IBADA YA USHIRIKA WA JUMAPILI KANISANI**
**9.1.Hatua za Kufuata**

1. Kufungua kwa maombi
2. Sifa na kuabudu
3. Matangazo
4. Neno
5. Ushuhuda
6. Sadaka na kwaya
7. Kufunga kwa maombi

**10.0.IBADA YA USHIRIKA WA KATIKATI YA WIKI**
**10.1.Hatua za Kufuata**

1. Kufungua kwa maombi
2. Sifa na kuabudu
3. Ushuhuda
4. Neno
5. Sadaka/ Matangazo
6. Kufunga kwa maombi

**USHAURI WA MWISHO**

Huu ni Mwongozo tu. Unaruhusiwa kubadilisha ratiba ya ibada yeyote ili iweze kuingiliana na shughuli yako ilimradi kuwe na taratibu njema na mpangilio mzuri kwenye ibada maana Mungu wetu sio Mungu wa machafuko ( confusion) bali wa Amani- 1 Kor 14:33.

Mtume Paulo amelishauri Kanisa kuwa na mpangilio mwema- “ lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu”- 1 Kor 14: 40
Kwengineko muombe Roho Mtakatifu akusaidie.Mungu abariki na kuinua huduma yako. Shukrani nyingi kwa wote-Amina.

8. Cheti cha kuwekwa wakfu ( kama kiko)
9. Kutoa shukrani
10. Kufunga kwa maombi

## 6.0. IBADA YA KUONDOA NADHIRI

### 6.1. Hatua za kufuata

1. Kufungua kwa maombi
2. Matangazo
3. Sifa na kuabudu
4. Hotuba/ ushuhuda ( hasa kwa mhusika mkuu)
5. Neno- Maandiko ya kusaidia: Hesabu 21:2, Lk 17:11-20, Mhub 5:4-5, 2 Sam 7: 12, Hesabu 30:2
6. Sadaka maalum ya shukrani ( mhusika)
7. Maombi maalum kwa mhusika/ wahusika
8. Kutoa shukrani
9. Kufunga kwa maombi

## 7.0. IBADA YA KUWEKA WAKFU/ KUSIMIKA WAHUDUMU (ORDINATION)

### 7.1. Hatua za Kufuata

1. Kufungua kwa maombi
2. Matangazo
3. Sifa na kuabudu
4. Hotuba/ ushuhuda ( hasa kwa mhusika/wahusika)---wasifu (Historia)
5. Neno-maandiko yanayofaa yasomwe/ mahubiri/kuombewa/kutiwa mafuta
6. Sadaka- watu wote ( mhusika/wahusika- watoe sadaka za shukrani)
7. Kutoa shukrani
8. Kufunga kwa maombi

## 8.0.IBADA YA KUWEKA WAKFU KANISA

### 8.1.Hatau za Kufuata

**Nje ya Kanisa** - Kufungua Kwa Maombi
- Aliyechaguliwa atafungua kanisa tena atangaze kuwa kanisa limefunguliwa rasmi
- Watu waingie ndani

**Ndani ya Kanisa** - Sifa na Kuabudu
- Neno: k.m. Zab.84:1-2, 1 Nyakati 29:10-13, Warumi 16: 25-27
- Hotuba
- Maombi ya Kuweka Wakfu Kanisa



**<u>MAWAIDHA KUMI-wachungaji wana shughuli nyingi lakini zingatia:</u>**

1. **UWE MTAWALA**… panga watenda kazi, shughuli, fedha, gawanya madaraka.
2. **UWE NA MPANGILIO**… uwe na wakati kwa ajili ya hivi: kujifunza/masomo, maombi, jamaa yako, mazoezi ya viungo, kupumzika, kutembelea watu, kazi ofisini.
3. **UWE NA HURUM**A…. kuwagusa wengine: ni lazima wewe kwanza umguse Mungu uwe na sikio kwa ajili ya kusikia, moyo kwa ajili ya kusihi, na mkono wa kumfikia mtu.
4. **UWE NA JUHUDI**…toa fungu lako; huwezi kuwafundisha watu wengine kama wewe hufanyi.
5. **UWE NA MSISIMKO**… roho nzuri yenye furaha inaambukiza, inaonyeshwa katika watu wako, na itawavuta watu wengine.
6. **UWE MWAMINIFU**… kwa Mungu, kwa kanisa, kwa huduma, weka mambo ya kwanza katika nafasi ya kwanza; kazi nyingine yo yote lazima iwe ya pili.
7. **UWE MLINZI**….wa kundi, ukiwa macho sana kwa kuangalia wale wanyama wa mgawanyiko na mafundisho ya uongo; epukana na wivu na usengenyaji ambao huharibu.
8. **UWE MNYENYEKEVU**… katika roho;ukiwa tayari kutumika kwa mikono yako wakati inapotakiwa; Yesu alikuja kutumika sio kutumikiwa.
9. **UWE MHUSIKAJI**….. katika shughuli zote; vijana, wanaume, wanawake, kwaya, bila ya kutawala.
10. **UWE MWENYE HAKI**…..usiwe na upendeleo katika kuamua, usifuate upande mmoja, vitu vyote viwe sawa kwa watu wote; wapokee wote, kwa sababu watu wa aina nyingi ndiyo huunda kanisa.

## 1.0. IBADA YA UBATIZO WA MAJI MENGI

### 1.1 Hatua za Kufuata

Matayarisho yote yafanywe mapema na ibada pia. Halafu watu waende kwenye maji mengi:

1. Kukiri- hapo kando ya maji, kila mwenye kubatizwa anawezakutoa ushuhuda mfupi wa imani katika bwana Yesu Kristo.
2. Maombi- maombi ya jumla kwa ajili ya watuwote wanaobatizwa na kwa ajili ya ibada hiyo kuwa ushuhuda kwa wote watakaohudhuria.
3. Kuingia kwenye maji- kwanza mchungaji, kisha wale wanaobatizwa, kwamstari, wakati washirika wengine wanaimba pambio. Tena mchungaji atamzamisha mmoja baada ya mwingine kwa utaratibu.
4. Maneno ya ubatizo( mchungaji aseme) - " ndugu/ dada ……………. Baada ya kukiri imani yako katika Bwana Yesu Kristo kuwa ni mwokozi wako, ninakubatiza katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.( Mzamishe mwili wote ndani ya maji, kisha umtoe.)
5. Wasaidizi- hawa watawasaidia waliobatizwa wakati wanapotoka kwenye maji, huku wakiongoza pambio wakati wa ibada nzima.
6. Kufunga kwa maombi.

## 2.0. IBADA YA MEZA YA BWANA

### 2.1. Hatua za Kufuata

1. Kufungua kwa maombi
2. Matangazo
3. Sifa na kuabudu
4. Neno- toa neno fupi juu ya maana ya Meza ya Bwana. Vifungu saidizi: 1 Kor 11: 23-30, Mt 26:26, 1Kor 10: 16, 1Pet 2:24, Waeb 9: 7-14.
5. Wasaidizi watumike- mchungaji awaandae hawa kwa kuwafundisha jinsi ya kuandaa meza na kuhudumu. Kisha awaelekeze lakufanya.
6. Mkate- soma maandiko kama Mt 26:26 kuhusu mkate. Hubiri kwa ufupi kisha watu washiriki kwa pamoja baada ya kutafakari.
7. Kikombe- soma maandiko kama Mt 26: 27-28 kuhusu kikombe. Hubirikwa ufupi kisha watu washiriki kwa pamoja baada ya kutafakari.
8. Maombi ya pamoja
9. Kufunga kwa maombi.



7. Kuona mwili na kutoa sadaka za faraja
8. Msafara kuelekea kaburini
9. Kwenye kaburi- kabla ya kushusha sanduku katika kaburi , mchungaji anasimama mbele ya kaburi na kusoma mojawapo ya maandiko yafuatayo kwa ufupi: 1 Kor 15:51, Yoh 11: 25-26, Yoh 14: 1-3, 27 Zaburi 103: 1-4; 13-18. Ufu 14:13
10. Maombi mafupi
11. Kuteremsha mwili kwenye kaburi, tena mtumishi aseme:

"Kama vile ilivyompendeza Baba yetu wa Mbinguni, katika mpango wake wa busara, kujichukulia kwake mwenyewe roho ya huyu marehemu, sisi tunauzika mwili wake katika udongo: mchanga kwa mchanga, mavumbi kwa mavumbi, majivu kwa majivu, tukitazamia tumaini lenye baraka lile la kutokea kwa Mungu Mkuuu na Mwokozi wetu, Yesu Kristo, ambaye atautengeneza upya mwili , katika mfano wa mwili wake mwenyewe wa utukufu, kulingana na matendo ya nguvu zake kuu, ambazo kwa hizo yeye anaweza kuvitiisha vyote chini yake."

12. Kufukia kaburi. Tena mstari wa kumalizia- 1 Wathesalonike 4:13-18
13. Maombi kwa walioachwa
14. Maombi ya mwisho- Waebrania 13: 20-21

## 5.0. IBADA YA KUOMBEA WATOTO

### 5.1. Hatua za Kufuata

1. Kufungua kwa maombi
2. Matangazo
3. Sifa na kuabudu
4. Neno fupi- Maandiko ya kusaidia: Mk 10:13-16, Mt 19:13-15, Mith 22:6, Mwan 18:19, Kumb 6:6-7, 1 Sam 1:20,24-28.
5. Wazazi wamlete mtoto mbele
6. Mchungaji atawauliza wazazi: Ninyi wazazi wa huyu mtoto, ni mapenzi yenu kumweka kwa Bwana?

***Jibu:*** ndio.

Mchungaji (aendelee): Mtaweka nadhiri ya kwamba mtamlea mtoto huyu katika kicho namafundisho ya bwana na kwamaneno yenu na matendo yenu kwamba mtamwongoza katika njia za Bwana kutoka utoto wake?

Mchungaji atamchukuwa mtoto mikononi mwake au amwekelee mikono akiwa na wazazi wake, tena atamwita mtoto kwa jina akisema:

…………………………, kufuatana na mapenzi ya wazazi wako, sasa nakuweka kwa Bwana katika jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Amina.

7. Kumuombea mtoto na kumrudisha kwa wazazi wake

Kristo Bwana wetu. Amina.

**Hatua ya Nne- Kuwaunganisha ,Kuwaombea na Kuwatangaza Rasmi**

***Mchungaji:*** (Tangazo- Mchungaji awashike mikono yao ya kulia awaunganishe, huku akisema):Kwa kuwa……………. na…………………… wamekubaliana pamoja machoni pa Mungu na mashahidi hawa, na wameahidiana upendo wao usiokwisha na uaminifu kwa kila mmoja, mimi kwa mamlaka niliyopewa kama mtumishi wa injili, natangaza kwamba wao ni mume na mke, kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Na alichounganisha Mungu, mwanadamu asitenganishe- Amina.

***Mchungaji:*** (Maombi- Maharusi wanapiga magoti ***nawachungaji wanaweka mikono juu yao kuwabariki***, kisha wakisimama, wanageuka na kuangalia mkutano)
***Mchungaji:***Nipeni ruhusa ya kuwajulisha kwenu Bwana na Bibi…………………..Na Mungu aibarilki jamii hii mpya kabisa- kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Amen.

**Hatua ya Tano- Kuweka Sahihi Vyeti**

***Mchungaji:*** **(Awaelekeze kuweka sahihi kwenye vyeti na wakisha maliza amuulize bibi arusi kuhifadhi vyema cheti chao)**

**Hatua ya Sita- Kumaliza: Kutoa Shukrani na Kuomba**
**Baada ya haya yote Mchungaji atoe shukrani zake za heri njema kwa wote na maharusi kwa kifupi tu, kisha arudishe mkutano kwa mwendeshaji wa ratiba ya siku hiyo-- mchungaji anaweza kufanya ombi fupi kabla atoke.**

6. Kumalizia kwa maombi.

## 4.0. IBADA YA MAZISHI
### 4.1. Hatua za Kufuata

1. Kufungua kwa maombi
2. Matangazo
3. Sifa na kuabudu
4. Historia ya marehemu
5. Hotuba
6. Neno



## 3.0. IBADA YA NDOA
### 3.1. Hatua za Kufuata

1. Kufungua kwa maombi
2. Matangazo
3. Sifa na kuabudu
4. Neno fupi
5. Kasisi aendelee kuanzia hapa -ndoa yenyewe:

**Hatua ya Kwanza- Utangulizi: Kujitambulisha na Kuleta Maharusi**
Mchungaji ajitambulishe tena aombe halafu aendelee nakufunganisha ndoa. Ikiwezekana achukuwe muda mchache katika shughuli hii yote bila kuwa na maneno mengi.
***Mchungaji:***Nani amletaye mvulana aweze kuunganishwa na mwanamke huyu? (waitikie -***ni sisi***- halafu waje mbele na kusimama pamoja na mvulana wao.)
***Mchungaji*** :Nani amtoaye msichana ili aweze kuunganishwa na mwanamume huyu? (waitikie -***ni sisi***- halafu waje mbele na kusimama pamoja na msichana wao.)
***Mchungaji:*** Nawaomba kwa rehema za mwenyezi Mungu mmkabidhi msichana wenu kwa mwanamume huyu rasmi)--------- Wazazi wa mvulana wamsaidie kupokea.

(Mchungaji anaweza kuwapatia nafasi fupi wazazi waongee halafu warudi na kukaa chini, tena Mchungaji aendelee)
**Bwana harusi ahakikishe kama ndiye mkewe au la-amfunue uso**
**Maharusi waachiliane mikono.**
***Mchungaji:*** Basi wapendwa, tumekusanyika hapa pamoja, mbele ya Mungu na mbele ya hawa mashahidi, ili kuunganisha mwanamume huyu na mwanamke huyu katika ndoa Takatifu, na kuwaingiza katika hali yao mpya kwa maombi yetu na salamu za kikristo. Ndoa, ambayo ni taasisi ya zamanizaidi katika dunia, ilisherehekewa mara ya kwanza katika bustani ya Edeni, wakati Mungu aliposema, ' si vyema mtu huyu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.” Ndoa ndio furaha moja tu ya Edeni ambayo imeweza kuendelezwa hadi leo hii, na huendelea kufariji, kujali, na kumaliza zile huzuni za hali zetu ya kuanguka.Bwana wetu Yesu aliweka muhuri wa kukubali kwake kwenye muungano huu wa kidunia kwa kuwapo kwake katika ndoa huko Galilaya, na huko akitenda muujiza wake wa kwanza uliowahi kuandikwa. Mtume Paulo alilinganisha ndoa na uhusiano kati ya Kristo na Kanisa lake, kuwa ni wa umoja mzuri, utunzaji wa hali nzuri, na kujitolea kwa upendo, hata mpaka kufa. Paulo alisema kuwa ni kitu cha kuheshimiwa na cha kufaa kwa watu wote, na sio cha kuingia bila mashauri au kwa urahisi tu, bali kwa heshima, kwa kufikiria, na hata kumcha

Mungu.Maandiko yanashikilia kiapo hiki cha ndoa kuwa ni kitu kitakatifu, na ni agano lenye kufunga na ambalo limekamilika kabisa. Nabii Malaki anasema hivi: Mtu yeyote asimtende vibaya mke wa ujana wake, kwa maana Bwana Mungu wa Israeli anasema kwamba hapendezwi na kuachana. Kwa hivyo, kile ambacho Mungu ameunganisha,mwanadamu asitenganishe.

**Hatua ya Pili- Maswali na Kiapo**

***Mchungaji:*** Ndugu…………………………………… je, wampokea mwanamke huyu awe mke wako wa ndoa, ukiahidi kumpenda, kumlinda na kumtunza tangu sasa, hadi kifo kitakapowatenganisha?

***Bwana Arusi:*** Ndivyo nitakavyofanya.

***Mchungaji:*** Dada…………………………………… je, wampokea mwanamume huyu awe mume wako wa ndoa, ukiahidi kumpenda, kumstahi na kumtii tangu sasa, hadi kifo kitakapowatenganisha?

***Bwana Arusi:*** Ndivyo nitakavyofanya.

**Wenye kuoana sasa washikane mikono ya kulia -Mchungaji aanze naBwana Arusi**

***Bwana Arusi:***Mimi……………… nakutwaa wewe………….. kuwa mke wangu ,niwe nawe tangu hivi leo na baadaye, kwa mema na mabaya, katika utajiri na umaskini, wakati wa ugonjwa na wakati wa uzima, nikupende, nikuhifadhi na kukuheshimu katika Bwana, hadi kifo kitakapotutenganisha, kwa amri takatifu ya Mungu, na kwa hiyo nakupa yamini yangu- Amina.

***Bibi Arusi:***Mimi……………… nakutwaa wewe………….. kuwa mume wangu ,niwe nawe tangu hivi leo na baadaye, kwa mema na mabaya, katika utajiri na umaskini, wakati wa ugonjwa na wakati wa uzima, nikupende, nikuhifadhi na kukuheshimu katika Bwana, hadi kifo kitakapotutenganisha, kwa amri takatifu ya Mungu, na kwa hiyo nakupa yamini yangu- Amina.

**Hatua ya Tatu- Kuvalishana Pete ( swali, kuonyesha pete na kuvalishana)**

***Mchungaji:***Ni kwa ishara gani mnaonyesha kwamba mtazishika nadhiri zenu kwa uaminifu?

***Pete zinatolewa tena Mchungaji anashika moja akisema:***Tazameni mfano wa pete hii: ni mzunguko usio na mwisho wa kitu cha thamani, pete ni mfano wa sifa zilizo bora zaidi za ndoa, matumaini, na umoja, ambazo huendelea bila ya kuvunjika mpaka kifo.

***Mchungaji akimuelekea Bwana Arusi, anasema:***Ndugu ………………………….hivi ndivyo unatakiwa kumzunguka mkeo katika maisha yake kwa nguvu za faraja na



upendo wenye kulinda na kumtunza.

***Mchungaji:***( Kwa wote wawili anasema: ) Na nyote mtimize ule mzunguko kamili wa wajibu na kupendana ambavyo huwafanya ninyi kuwa kitu kimoja katika makusudi yenu na katika roho.”-----------------------Maombi mafupi ya kuombea pete kisha wavishane.

**Kuweka pete**

***Bwana Arusi:***(Anaweka pete kwenye kidole cha Bibi Arusi na akiwa ameishika, anasema)Mimi…………………….ninakupa wewe……………..…pete hii, kama ishara ya kwamba wewe ni mke wangu niliyekuchaguwa, nami nitakupenda, nitakuheshimu, nitakutunza na kukushirikisha mambo yote niliyo nayo na nitakayopata baadaye, katika siku zote za maisha yangu. Kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Amina.

***Bibi Arusi :***(Naye atasema)Mimi…………………….ninakupa wewe……………..…pete hii,kama ishara ya kwamba wewe ni mume wangu niliyekuchaguwa, nami nitakupenda, nitakuheshimu, nitakutii na kukushirikisha mambo yote niliyo nayo na nitakayopata baadaye, katika siku zote za maisha yangu. Kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Amina.

**Maharusi wanashikana mikono ya kulia**

***Mchungaji:*** (Akimwambia Bwana Arusi) Ndugu…………………….., mtunze vyema mwanamke huyu maana sasa anajikabidhi katika ulinzi wako, na ujitahidi sana kuishi katika Bwana kiasi cha kwamba hakutakuwepo na neno lo lote au tendo ambalo litamfanya yeye kuumia au kulowa macho yake kwa machozi.

***Mchungaji:*** (Akimwambia Bibi Arusi) Dada……………………………….jitahidi sana kwa ungwana wako, moyo huo ambao umeupata kutokana na uzuri wako kumtii mume wako katika Bwana.

***Mchungaji:*** (Akiwaambia wote wawili): Msiruhusu sauti zenu kupoteza sauti zile laini za upendo, wala macho yenu kusahau mwanga mzuri, wala vipaji vya nyuso zenu kuacha kuwa nuru ile iliyokuwepo katika siku za uchumba wenu, katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu-Amina.

***Mchungaji:*** (Maombi): Ee Mungu wa milele, muumbaji na mwenye kuhifadhi wanadamu wote, mtoaji wa neema za kiroho zote, tuma baraka zako juu ya hawa watumishi wako, ili waweze kutenda kwa uhakika na kushika agano lile kati yao, ambalo pete hii ni ishara yake na ni ahadi, tunaomba upendo kamili na amani ya kudumu viwe ni sehemu yao wakati watakapoishi kulingana na sheria zako, kwa Yesu